

Mikakati ya Urekebu wa Kiswahili kama Lugha Rasmi Nchini Kenya

*Modgen Chisia*¹

Chuo Kikuu cha Nairobi

*Iribe Mwangi*²

Chuo Kikuu cha Nairobi

*Ayub Mukhwana*³

Chuo Kikuu cha Nairobi

na

*Hezron Mogambi*⁴

Chuo Kikuu cha Nairobi

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.2>

Ikisiri

Makala haya yanajadili jinsi Kiswahili kilivyokubalika kama lugha rasmi nchini Kenya baada ya kuidhinishwa kwa Katiba ya 2010, na maswali yaliyoibuka kuhusu uwezo wake katika mawasiliano rasmi, hasa ikilinganishwa na Kiingereza. Lengo la utafiti lilikuwa kubainisha mikakati ambayo Kiswahili kinatumia kukua na kufanikisha mawasiliano rasmi. Data ilikusanywa kutoka kwa maandishi mbalimbali na *Kamusi Pevu ya Kiswahili* (2016). Utafiti huu uliozaa makala haya ulionesha kwamba Kiswahili kinatumia mikakati ya urekebu wa kifonolojia na kisemantiki kupata msamiati na istilahi za kufanikisha mawasiliano. Utafiti unapendekeza kuundwa kwa chombo cha kitaifa kusimamia maendeleo ya msamiati wa Kiswahili na kupendekeza Kiswahili kiweze kutumika katika mawanda yote, yakiwemo rasmi, ili kiweze kufanikisha majukumu yake mapya. Aidha, makala haya yanapendekeza kuwa Kiswahili kinastahili kutumiwa katika mawanda yote ili kiweze kurekebu na kuyafanikisha majukumu yake mapya ya kimawasiliano kama lugha rasmi nchini Kenya.

1.0 Utangulizi

Ili lugha ya Kiswahili iweze kutumiwa kuyatekeleza majukumu yake mapya kama lugha rasmi nchini Kenya, haina budi kurekebu. Urekebu wa lugha ni utaratibu

¹ Barua pepe: chisiauonbi.ac.ke@students.uonbi.ac.ke

² Barua pepe: iribe@uonbi.ac.ke

³ Barua pepe: ayubmukhwana@yahoo.com

⁴ Barua pepe: Hezron.mogambi@uonbi.ac.ke

wa kimakusudi au unaotokea kiasilia wa kuifanyia lugha mabadiliko ili iweze kuyatekeleza majukumu yake mapya ya kimawasiliano (Coulmas, 1989). Urekebu unaofanywa kimakusudi hutekelezwa katika vikao vinavyoandaliwa na watumiaji lugha, hasa wataalamu wa lugha ilhali wa kiasilia hutokea tu bila vikao vyovyote vya wataalamu wa lugha. Lugha ya Kiswahili inatumia mikakati mbalimbali ya urekebu nchini Kenya ili iweze kutumiwa kama lugha rasmi. Katika utafiti huu tulijadili matumizi ya Kiswahili pamoja na ukopaji na utohozi.

2.0 Utaratibu wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kusoma maandishi mbalimbali kuhusu urekebu wa lugha pamoja na matumizi. Katika kutimiza lengo la kuchunguza urekebu wa msamiati na istilahi zinazokopwa na kutoholewa katika lugha ya Kiswahili, uchunguzi huu ulibainisha msamiati uliokopwa kutoka lugha za Kiingereza, Kiarabu, Kihindi, Kireno, Kiajemi na Kijapani. Aidha, baada ya kubainisha msamiati huo, *Kamusi Pevu ya Kiswahili* (2016) ilitumiwa kubainisha maana na asilia ya msamiati huo. Aidha, *Cambridge English Dictionary* pamoja na *Google Translate* zilitumiwa kubainisha maana na tafsiri za baadhi ya leksikoni kutoka lugha za Kiingereza, Kihindi, Kijapani, Kiarabu na Kireno.

3.0 Nadharia Iliyotumiwa

Utafiti uliozaa makala haya ulifanywa kwa msingi wa Nadharia ya Saikolojia ya Kijamii (kuanzia sasa NSK) iliyoasisiwa na Lambert mwaka 1967. Nadharia hii inazingatia hisia za mtu binafsi katika kujifunza na kutumia lugha ya pili (kuanzia sasa L2) au lahaja fulani. Kulingana na NSK, kasi ya mtu kujifunza lugha ya pili inaongozwa na hisia au mtazamo wake kwa jamiilugha husika. Iwapo mtu ana mtazamo chanya kuhusu jamiilugha fulani, ikiwa ni pamoja na kuvipenda na kuvitathmini vipengele vyote vya jamiilugha hiyo, basi ujifunzaji wake lugha husika huwa wa kasi ya juu. Kwa upande mwingine, mtazamo hasi wa mtu kuhusu vipengele vya jamiilugha fulani humaanisha mtazamo hasi kwa lugha ya jamiilugha hiyo, hali inayokwaza ujifunzaji wa kasi na hata matumizi ya lugha hiyo (Lambert, 1967; Wamalwa, 2020; Mukhwana, 2023).

NSK inabainisha aina mbili za hamasa zinazoongoza ujifunzaji L2 au lahaja pamoja na matumizi yake: hamasa ya kujumuishwa na hamasa ya kiutekelezaji (Gardner na Lambert, 1972). Hamasa ya kujumuishwa hudhihirika kupitia nia na ari ya mjifunzaji L2 au lahaja kutaka kutambuliwa na kuthaminiwa kama mshirika kindakindaki wa jamiilugha husika. Mjifunzaji lugha kwa kuongozwa na aina hii ya hamasa huwa na ufanisi wa hali ya juu kwa kuwa anataka kujinasibisha na kujitambulisha na jamiilugha ya lugha ambayo anajifunza kwa kuwa anavipenda vipengele vya jamiilugha hiyo ikiwa ni pamoja na utamaduni wake (Mukhwana, 2023; Samada, 2012).

Hamasa ya kiutekelezaji inamwongoza na kumchochea mtu anayejifunza L2 au lahaja fulani kwa nia za kujifaidi kiuchumi, kupita mitihani au kupata nafasi za ajira au mamlaka fulani. Kwa hali hii, mtu kama huyo huwa amewekewa sharti la kujua L2 au lahaja fulani ndipo anufaike (Gardner na Lambert, 1972; na Mohamed, 2005). Maadamu msukumo wa mtu kama huyo hautokani na haja ya kutambuliwa kama mmoja wa wanajamii husika, kasi yake ya kujifunza L2 na hata matumizi yake huwa ya chini mno.

Kama anavyotambua Mukhwana (2008), Ryan, Giles na Sebastian (1982) walijitokeza na mkabala jumuishi na ambao unazingatia thamani ya kitaashira ya lugha katika jamii ya uwililugha au wingilugha kama Kenya. Mkabala huu unajumuisha mikabala midogo inayozingatia vigezo vingine vya kujifunza na kutumia lugha. Mkabala mdogo wa kwanza unahusisha uthabiti na usanifishaji ilhali wa pili unahusisha mitazamo ya hadhi na tathmini ya mshikamano wa jamiilugha.

Mkabala mdogo wa uthabiti na usanifishaji unabainisha kwamba lugha zilizosanifishwa pamoja na zile zinazotumiwa na watu wengi kikanda au kimataifa huwa zimekwezwa kihadhi na huvutia idadi kubwa ya wazungumzaji kuliko zile ambazo hazijasanifishwa. Lugha zitumiwazo na watu wengi kwa mawasiliano mapana hupata uthabiti wake kwa sababu ya thamani za kitaashira ambazo zinahusishwa nazo. Kitaashira lugha zinazotumiwa katika mawanda muhimu kama sheria, bunge, vyombo vya habari, utawala wa serikali na kuendesha shughuli za elimu huonekana kuwa zenye hadhi ya juu (Musau 2002; Mukhwana, 2008)

Mkabala huu huzingatia pia nafasi ya watumiaji wa lugha pamoja na asasi muhimu zinazohusika katika uimarishaji na usanifishaji lugha (Ojwang, 2011). Kipengele hiki kiliufaa utafiti huu kwa kuzingatia asasi kama vile vyombo vya habari na za elimu katika kuendeleza urekebu wa Kiswahili nchini Kenya.

Mkabala mdogo wa mitazamo ya hadhi na tathmini ya mshikamano wa jamiilugha hueleza ruwaza za upendeleo wa watu katika kutumia lugha. Watu wengi hupendelea kutumia lugha ambazo zina hadhi kuu katika jamii zao. Lugha hizo ni zile zilizosanifishwa na zenye utumiaji mpana katika jamii (Mukhwana, 2023).

4.0 Matumizi ya Kiswahili nchini Kenya

Kutumia lugha ni miongoni na mikakati muhimu ya kusaidia urekebu wake. Obonyo (1999) anaeleza hali hii vyema kama anavyonukuliwa na Okombo (2001), kwa kutaja kwamba, lugha hukua na kuimarika kwa mawasiliano kadiri itumiwavyo. Matumizi hayo yanastahili kuyahusisha mawanda yote yakiwamo yale ya elimu, biashara, utawala, siasa, bunge, sheria, teknolojia, utafiti na michezo. Lugha hukua kutokana na kukabiliana na changamoto za kimtindo, kimsamiati, kiistilahi na mahitaji ya sajili za miktadha mbalimbali na ndipo inapopata uthabiti wa kimawasiliano.

Hali hii inaafikiana na hitimisho la Strongman (2017) anayechunguza kuchipuka kwa lahaja mbalimbali katika Kiingereza cha *New Zealand* kwa kutumia nadharia ya Trudgill. Strongman (2017) anaitumikisha mikakati ya hisabati na kubainisha kuwa kuchipuka huko kwa lahaja mpya katika Kiingereza cha *New Zealand* kunatokana na kutumia lugha hiyo kwa wingi pamoja na umoja wa jamiilugha. Fauka ya kubainisha umuhimu wa mambo kama hadhi pamoja na utambulisho wa watumizi wake, Trudgill (2004) anaeleza jinsi lahaja zinavyoweza kuchipuka katika lugha kutokana na wingi wa matumizi ya lugha husika. Aidha, mitindo mipya ya kimawasiliano, msamiati mpya pamoja na istilahi huweza kuchipuka ili kuiwezesha lugha kutimiza mahitaji muhimu ya kimawasiliano.

Kadiri lugha ya Kiswahili inavyoenea kimatumizi na kijiografia na kupata lahaja mbalimbali, ndivyo inavyokua na kuimarika na kwa hivyo kuwa katika hali ya kuweza kufanikisha mahitaji yake mapya ya kimatumizi kama lugha rasmi nchini Kenya. Coulmas (1989) na Musau (2002) wanaeleza kwamba kuipa lugha majukumu mapya hakuifanyi kurekebu na kuwa tayari kwa majukumu hayo, bali urekebu huo unatokana na kutumiwa katika mawasiliano ya kila mara katika mawanda yote ya kijamii. Ni bayana kwamba matumizi ya Kiswahili katika elimu kama somo la lazima katika shule za msingi na za upili, hasa kuanzia mwaka wa 1985 kufuatia mapendekezo ya Tume ya Mackay, yamechangia kuenea na kukua kwake katika misingi ya msamiati, istilahi na mitindo mbalimbali ya kimawasiliano. Uamuzi huo ulileta mapinduzi makubwa katika mfumo wa elimu na kuchangia kukua kwa machapisho ya vitabu vya kiada, vitabu vya fasihi na makala kwa Kiswahili ili kukidhi mahitaji ya shule na vyuo. Aidha, idadi ya wanafunzi wanaosomea somo la Kiswahili katika vyuo vikuu ilikua ili kufundisha katika shule za upili (Ministry of Education, 2002; Michira 2014; Mungania, 2014; Oduor na Timammy 2016; Krezer na Oluch-Sule, 2022) Uamuzi mwingine muhimu uliofanywa na Taasisi ya Kukuza Mitaala ya Kenya ni kufanya Kiswahili somo la lazima katika sekondari ya upeo huku idadi ya vipindi vyake ikiwiana na vya Kiingereza. Ingawaje Kiingereza bado kinatumiwa kama lugha ya kufundishia katika viwango vyote vya elimu katika Mtaala wa Elimu ya Kiumilisi, hatua hiyo inaonesha nia ya kukiwezesha Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya (Kenya Institute of Curriculum Development, 2024). Kupendelewa kwa Kiingereza zaidi ya Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Kenya kunatokana na hamasa ya kiutekelezaji. Hii ni kwa kuwa watu wengi, ikiwa ni viongozi wanaofanya maamuzi kuhusu elimu, wanakihusisha Kiingereza na fursa nyingi za kiuchumi, masomo, kupanda cheo kitaaluma na matumizi ya kimataifa kuliko Kiswahili.

Kama lugha nyingine asilia za bara Afrika, lugha ya Kiswahili inakabiliwa na tatizo la wakati na katika mazingira ya sasa ya sayansi na teknolojia. Matokeo mengi ya kivumbuzi yanatoka katika mataifa ya Kimagharibi na kuingizwa kwa Kiswahili kupitia Kiingereza. Kwa hali hii, lugha ya Kiswahili, kama nyinginezo za bara Afrika, inakuwa katika harakati ya kupata msamiati na istilahi za dhana

hizo. Hata hivyo, kadiri dhana hizo za Kimagaribi zinavyoingizwa katika utamaduni wa Kiafrika, ndivyo Kiswahili kama lugha nyinginezo, kinavyojikakamua kupata msamiati na istilahi za kuzitajia (Madiba, 2000; Mungai, 2011; na Okombo, 2001).

Hali inayokikumba Kiswahili si ya kipekee kwa Kiswahili kwani hata lugha za Kimagharibi kama vile Kijerumani ziliwahi kukabiliwa na changamoto hiyo kufikia karne ya saba. Lau kama hapangefanywa juhudi za makusudi kuitumikisha lugha hiyo katika mawanda yote ya kimawasiliano, yakiwamo yale rasmi; lugha hiyo isingerekebu na kuwa miongoni mwa lugha zenye hadhi kubwa ulimwenguni kama vile Kifaransa na Kiingereza hasa katika bara la Ulaya (Coulmas, 1989). Utafiti huu unatambua umuhimu wa Kiswahili kutumiwa sambamba na Kiingereza kama moja kati ya mikakati muhimu ya urekebu wake.

Webb na Kembo-Sure (2000), wanaonukuliwa na Okombo (2001), wanatambua majukumu mawili muhimu ya lugha katika jamii inamotumiwa: jukumu la uamilifu, na jukumu la kitaashira. Kwa upande wa kitaashira, lugha hutumiwa kuyatambulisha na kuyatofautisha makundi ya watu katika jamii. Jukumu hili ni kama lile linalotekelezwa na bendera au wimbo wa taifa katika taifa fulani. Watu wanaozungumza lugha moja hubainika kama wamoja na tofauti na wengine wanaozungumza lugha tofauti duniani. Hali hii huwa muhimu mno iwapo lugha imekwezwa hadhi kuwa lugha ya taifa au rasmi na kutumiwa katika mawanda mapana na mengi ya kimawasiliano katika jamii.

Okombo (2001) anayabainisha mambo matatu makuu ambayo lugha huyafanikisha katika kutekeleza dhima yake ya utendakazi. Mambo hayo ni: kwanza, dhima ya kuarifu: katika kutimiza hili, lugha hutumiwa kama chombo cha kuwasilisha na kupokea taarifa, matamano pamoja na hisia za wanadamu. Pili, ni dhima ya kubagua na kujumuisha: hapa lugha hutumiwa kama msingi wa kujinasibisha na kikundi fulani cha watu na wakati huohuo kujibaidisha na vikundi vingevyo vya watu. Hatimaye ni dhima ya kushirikisha: hapa lugha hutumiwa kama chombo cha kuwawezesha wanakikundi fulani kushirikiana katika shughuli ya kijamii na kunufaika kutokana na mambo yanayowabainisha kama wamoja. Dhima hizi zinaweza kutekelezwa tu na Kiswahili iwapo kitapata fursa za kimatumizi katika nyanja zote nchini Kenya.

Katika Bunge la Taifa, ingawaje Kanuni za Kudumu zimetafsiriwa kwa Kiswahili, na Alhamisi kutangazwa kama siku ya mijadala kuendeshwa kwa Kiswahili, matumizi yake ni machache mno. Ni wabunge wachache mno, hasa wa kutoka maeneobunge ya pwani ambao hutumia Kiswahili bungeni mara kwa mara (Parliament of Kenya, 2022).

Matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari pia ni finyu ikilinganishwa na Kiingereza. Vipindi vingi, taarifa za habari na matangazo mengi hupeperushwa kwa Kiingereza katika redio na runinga. Isitoshe, baadhi ya vipindi hutumia mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza au hata Sheng' huku baadhi ya watangazaji wakitumia Kiswahili kilichoborongwa kwa nia za ucheshi (Mwaliwa, 2014). Kuwapo kwa gazeti moja tu linalochapishwa kwa Kiswahili (*Taifa Leo*) huku mengine yote yakichapishwa kwa Kiingereza ni ishara ya matumizi finyu ya Kiswahili katika magazeti nchini Kenya. Hata hivyo, jambo linalotia moyo ni kwamba usomaji wa gazeti hilo la *Taifa Leo* unaimarika huku ule wa magazeti ya *Daily Nation* na *The Standard* ukipungua kwa kuzingatia takwimu za mwaka 2021 na 2022 kama inavyobainika katika jedwali hapa chini (Media Council of Kenya, 2022):

Jedwali Na. 1: Takwimu za Usomaji Gazeti la Kiswahili la *Taifa Leo* Nchini Kenya

Gazeti	Lugha Inayotumika	2021	2022	Mkengeuko
<i>Daily Nation</i>	Kiingereza	59%	53%	-6%
<i>The Standard</i>	Kiingereza	28%	22%	-6%
<i>Taifa Leo</i>	Kiswahili	0.20%	15%	14.8%

Kama inavyojitokeza katika Jedwali Na. 1 hapo juu, usomaji wa gazeti la *Taifa Leo* uliimarika kutoka mwaka wa 2021 hadi 2022 kwa asilimia 14.8 huku ule wa *Daily Nation* na *The Daily Standard* ukipungua kwa asilimia 6 katika kipindi hicho. Hii ni ishara kwamba Kiswahili kama lugha kinaendelea kupanuka kimatumizi katika magazeti nchini Kenya.

Lugha ya Kiswahili inaweza tu kurekebu kwa kutumiwa katika mawanda yote ya mawasiliano nchini Kenya, yakiwamo yale rasmi na hatimaye kutumika kikamilifu kwa pamoja na Kiingereza ambacho kimejivunia ukiritimba wa kimawasiliano rasmi tangu mkoloni Mwingereza alipoingia nchini Kenya. Hali hii ya Wakenya wengi kutumia Kiingereza kwa wingi inachochewa na sababu za kiutekelezaji kwa kuwa wanahusisha lugha ya Kiingereza na nafasi nyingi muhimu za kiusomi na kiuchumi, huku Kiswahili kikihusishwa na masuala kama vile uzalendo. Kwa wanaotumia Kiswahili, msukumo wao ni haja ya kujumuishwa na kujitambulisha na uzalendo unaofungamana na dhana kwamba Kiswahili ni lugha asilia na wanaona fahari kuitumia badala ya Kiingereza ambayo ni lugha ya kigeni.

5.0 Upanuzi wa Msamiati Kupitia Ukopaji na Utohozi

Urekebu wa lugha hufungamana na utaratibu wa kuipa lugha hiyo usasa. Kuipa lugha usasa huhusisha utaratibu wa kuipa msamiati, istilahi pamoja na mitindo ya kuiwezesha kuyakimu mawasiliano yote, yakiwamo yale rasmi. Utaratibu huu unaweza kufanywa kwa kutumia rasilimali za ndani ya lugha husika au kutoka

kwa lugha zinazotagusana nayo katika mawasiliano (Daswani, 1989; Ferguson, 1977; Madiba 2000). Baadhi ya wataalamu wametaja utaratibu wa kuongeza msamiati na istilahi katika lugha fulani kwa kuichota kutoka kwa lugha nyinginezo kama utaratibu wa kuichafua na kuiondolea uasilia (Ferguson, 1977; Jermud, 1977; Okombo, 2001; na Mungai, 2011). Mkondo huu wa mawazo unakosa kutambua kwamba hapana lugha inayojitegemea duniani. Lugha ni kitu hai ambacho hukua kwa kutangamana na nyinginezo. Kwa sababu hii, haihalisi lugha fulani kukua na kuwa na uwezo wa kupata msamiati na istilahi za kutaja dhana na tamaduni mpya bila kukopa kutoka kwa jamiilugha inazotangamana nazo. Monitor (2017) inatambua kwamba ili kukidhi mahitaji ya kila siku ya kimawasiliano, uundaji wa maneno hutokea kila mara kote ulimwenguni kiasi kwamba neno moja huundwa ulimwenguni kila baada ya dakika tisini na nane.

Sehemu ifuatayo inazingatia urekebu wa Kiswahili kupitia ukopaji na utohozi kama njia za kuongeza msamiati na istilahi.

5.1 Ukopaji na Utohozi

Ukopaji ni utaratibu wa kulihaliwisha neno la lugha chanzi hadi kwenda lugha pokezi ili kufidia upungufu wa kimawasiliano katika lugha hiyo. Ukopaji huenda sako kwa bako na utohozi ambapo neno linalokopwa hufanyiwa mabadiliko ya kisemantiki na ya kifonolojia ili liweze kuafikiana na mahitaji ya kiisimu ya lugha pokezi. Kwa kawaida, taratibu hizi mbili hufungamana na athari kwa msamiati na istilahi zinazokopwa kama vile upanuzi wa kisemantiki, ubanifu wa kisemantiki, uhamisho wa kisemantiki au hata udumishaji wa kisemantiki (Yule, 1996; Madiba, 2000; Petzell, 2005; Mwita, 2009; Iribemwangi na Mukhwana, 2011; Akida, 2013).

Katika lugha ya Kiswahili, ushahidi unabainisha kuwapo kwa udumishaji wa baadhi ya msamiati na istilahi zinazokopwa. Kwa mfano, maneno kama vile *piano*, *guru na kimono* yaliyokopwa kutoka Kiingereza, Kihindi na Kijapani mtawalia, yanadhihirisha udumishaji wa kiothografia na kisemantiki, tofauti ya pekee ikiwa katika utamkaji wake (Petzell, 2005; Akida, 2013; Wamitila, 2016).

Ukopaji wa msamiati na istilahi huzingatia siyo tu vigezo vya kiisimu, bali pia visivyo vya kiisimu. Vigezo vya kiisimu vinajumuisha mtagusano wa lugha pamoja na miundo ya kiisimu ya lugha husika. Lugha ya Kiswahili imekopa mno kutoka kwa lugha za Kibantu, Kiarabu na Kiingereza. Ukopaji kutoka lugha za Kibantu ulihusisha vipengele vya kitamaduni kwa wingi. Lugha hiyo ilikopa mno kutoka Kiarabu kuhusiana na vipengele vya kidini, kisheria, kilimo na utawala katika nyakati ilipotagusana na utamaduni wa Kiarabu, hasa katika kipindi cha kabla ya mkoloni Mwingereza. Baadhi ya watafiti wamebainisha kwamba Kiswahili kimekopa kati ya asilimia ishirini na thelathini ya msamiati wake kutoka Kiarabu (Mwita, 2009; Iribemwangi, 2012; Akida, 2013). Ukopaji kutoka

Kiingereza ulianza kukita mizizi katika kipindi cha ukoloni wa Mwingereza, mataifa ya Afrika Mashariki yalipokuwa chini ya himaya ya Malkia wa Uingereza. Hali hiyo imeendelea kudumu hasa katika enzi hii ambapo uvumbuzi wa teknolojia na sayansi huingizwa katika utamaduni wa Kiswahili kupitia kwa Kiingereza (Petzell, 2005; Njagi, 2011; Iribemwangi, 2012). Moja kati ya sababu za Kiswahili kukopa mno kutoka Kiingereza ni kwamba lugha hiyo ya Kiingereza ina msamiati wa kimataifa, hali inayosahilisha uhawilishaji wa msamiati huo kwa lugha nyingi ulimwenguni. Isitoshe, muundo wake wa kiisimu, kama lugha mahuluti, huwezesha msamiati wake kurekebu upesi na kwa urahisi unapoinzwa katika Kiswahili (Madiba, 2000; Njagi, 2011).

Masuala yasiyo ya kiismu ambayo huathiri ukopaji ni siasa na muktadha wa kihistoria, kiwango cha elimu cha watumiaji lugha pokezi na kiwango cha uwililugha katika jamiilugha pokezi pamoja na hadhi ya lugha chanzi. Siasa na muktadha wa kihistoria vinapendelea Kiingereza kuwa lugha chanzi kwa msamiati na istilahi zinazohawilishwa kwa Kiswahili. Mkoloni Mwingereza alikuwa na athari ya muda mrefu siyo tu katika siasa za Afrika Mashariki, bali pia kwa elimu, dini na vipengele vingine vingi vya maisha ya wenyeji. Aidha, hali hiyo ilikweza lugha ya Kiingereza kihadhi zaidi ya lugha asilia, ikiwamo Kiswahili katika mawanda ya elimu, sayansi, teknolojia, siasa na sheria miongoni mwa mengine mengi. Uelewa hapa ni kwamba, kwa kawaida, lugha zenye hadhi ya juu, huzikopesha kwa wingi lugha za hadhi ya chini kwa kuwa zina uwezo wa kushinikiza tamaduni zake kwa wenyeji na lugha zao zinazoonekana kuwa za hadhi ya chini (Batibo, 1996; Madiba, 2000; Iribemwangi, 2012).

Huku ukopaji ukisalia kuwa utaratibu maarufu wa kuunda msamiati katika lugha ulimwenguni, utaratibu huu una manufaa na hasara zake. Miongoni mwa manufaa yake ni kwamba ukopaji huipa lugha lengwa mguso wa kimataifa kwa kuwa istilahi za lugha za kigeni huweza kubainika katika mfumo wa lugha pokezi. Aidha, utaratibu huu husahilisha ubunaji wa msamiati na istilahi katika lugha pokezi kwa kufanyia maneno yanayokopwa marekebisho machache katika sauti na miundo yake. Upungufu unaohusishwa na utaratibu huu ni kuwa siyo rahisi kuunda msamiati zaidi kutokana na istilahi ambazo hazijatoholewa kikamilifu, mbali na kuifanya lugha pokezi kupoteza uasilia wake kwa kuwa istilahi za kigeni huzagaa ndani yake. Ni kutokana na hali hii ambapo wataalamu wa lugha kama Kiebrania na Kiswahili husisitiza mwelekeo wa uasilia wa kubuni msamiati na istilahi kutoka ndani ya lugha nyenza kiisimu au lahaja za lugha husika badala ya kukimbilia lugha za kigeni, na zenye miundo tofauti ya kiismu (Jermudd, 1977; Massamba, 1989). Kasoro ya ziada inayofungamana na utaratibu huu ni hatari inayotokana na utohozu wa istilahi mbili au zaidi tofauti za kutaja dhana moja katika lugha pokezi, hali inayoweza kutatiza uelewa katika lugha pokezi (Kevogo, 2011). Yamkini hii ndiyo sababu baadhi ya wataalamu wanapendekeza haja ya mbinu hii kutumiwa katika uundaji wa istilahi wala siyo msamiati wa nyanja zote. Hali hii itasaidia

kudumisha uasilia wa lugha pokezi kwa kiwango kikubwa kwani ni rahisi kuzibainisha istilahi katika lugha zote ulimwenguni kwa kuwa zina arki za umataifa (Iribemwangi na Mukhwana, 2011).

Mkabala wa uasilia unasisitizwa katika ukopaji wa msamiati na istilahi kutoka ndani ya lugha ya Kiswahili. Hali hii inaelekeza kwamba panapokuwa na haja ya kupata istilahi au msamiati wa kutaja dhana fulani, hatua ya kwanza ni kuzingatia lahaja za Kiswahili. Iwapo hapana suluhu, hatua ya pili ni kuzingatia rasilimali kutoka lugha za Kibantu. Hatua ya tatu na ya mwisho, ni kuzingatia lugha za kigeni (Jermudd, 1977; Massamba, 1989; Okombo, 2001). Ingawaj hili ndilo pendekezo linalotiliwa maanani na wapangaji lugha ya Kiswahili, ushahidi wa sasa unadhihirisha kwamba mkabala wa sera ya uhalisia wa utekelezaji pia unatumika katika lugha ya Kiswahili. Mkabala huu unatilia maanani umuhimu na uwezo wa utekelezwaji na matumizi ya istilahi na msamiati unaokopwa na kuingizwa ndani ya Kiswahili.

Kuhusu aina za maneno, nomino zinadhihirisha ushahidi mwingi wa ukopaji kuliko aina nyingine za maneno. Taswira hiyo inaafiki hitimisho la Winford (2003) anayenukuliwa na Iribemwangi (2013) akisema kwamba ngazi ya ukopaji katika lugha nyingi ulimwenguni huzipa nomino kipaumbele, kisha vivumishi, vitenzi, halafu aina nyinginezo za maneno. Katika lugha ya Kiswahili, nomino ndiyo aina ya maneno iliyokopwa zaidi kuliko aina nyingine za maneno. Aidha, inaelekea kwamba ukopaji mwingi katika kipindi cha sasa unahusu msamiati wa teknolojia, mawasiliano, sayansi, usafiri, elimu na nyinginezo. Sehemu kubwa ya msamiati na istilahi hizo inatoka katika lugha ya Kiingereza kwa uelewa kwamba, mbali na kuwa lugha ya hadhi ya juu, lugha hiyo ndiyo wenzu wa kuyapitisha maarifa na utamaduni katika nyanja hizo, siyo tu katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa jumla, bali katika nchi ya Kenya kimahususi (Petzell, 2005; Mwita, 2009; Akida, 2013; Iribemwangi, 2013).

Katika sehemu inayofuata, makala haya yalichunguza mikakati ya kiisimu inayofungamana na ukopaji na utohozi wa msamiati na istilahi katika lugha ya Kiswahili. Mikakati ya kiisimu inayozingatiwa hapa inahusu urekebu wa kifonolojia na urekebu wa kisemantiki.

5.1.1 Urekebu wa Kifonolojia

Maneno yanaweza kupata mabadiliko katika kiwango cha kifonolojia yanapokopwa na kuingizwa katika lugha pokezi. Mabadiliko hayo huhusisha sauti, silabi na toni. Hali hiyo itwayo urekebu wa kifonolojia hukusudia kuhakikisha kwamba msamiati mpya unawiana na na mfumo wa kifonolojia wa lugha pokezi (Madiba, 2000; Akida, 2013; Njagi, 2016). Utafiti huu uliijadili hali hii kwa kuzingatia msamiati na istilahi zilizokopwa kutoka Kiingereza, Kiarabu, Kireno, Kihindi na Kijapani.

Tafiti za wataalamu mbalimbali wa Kiswahili zinaonesha kwamba lugha ya Kiswahili ina kati ya konsonanti 23 na 27. Kufikia sasa hapaelekei kuwa na mwafaka wa idadi kamili ya konsonanti hizo huku wataalamu tofautitofauti wakibainisha idadi tofauti (Habwe na Karanja, 2004; Njogu na wenzake, 2006; Akida, 2009; Iribemwangi, 2010). Kulingana na tafiti hizo kuna jumla ya irabu tano katika Kiswahili: /a/, /ɛ/, /i/ /ɔ/ na /u/. Mfumo wa sauti za Kiswahili unatofautiana na mfumo wa sauti ya lugha ambazo Kiswahili kinakopa msamiati na istilahi zake. Kwa mfano, Kiingereza kina irabu zaidi ya 20 ilhali Kiarabu kina konsonanti 26 na irabu 6, 3 kati ya hizo ni irabu msingi, pamoja na nusu-bu 2. Kihindi kina jumla ya konsonanti 40 na irabu 13. Ingawaje baadhi ya sauti hizi hufanana na zile za Kiswahili, nyingine ni tofauti kabisa.

Fauka ya mfumo wa sauti, lugha ya Kiswahili ina muundo pendwa wa silabi wazi zinazoundwa kwa konsonanti na irabu na ziishiazo kwa irabu, tofauti na lugha kama Kiarabu na Kiingereza ambazo silabi zake aghalabu huwa funge (Akida, 2013; Habwe na Karanja, 2004; Iribemwangi, 2010; na Mwita, 2009). Aidha, lugha hii ya Kiswahili ina silabi mwambatano za konsonanti mbili au tatu. Sauti mwambatano za konsonanti mbili huundwa kwa nazali za midomo, ufizi na kaakaa gumu /m/, /n/ au /j/ mtawalia. Hali hii ni bayana katika maneno kama *mbali*, *ndege*, na *kunywa*. Silabi mwambatano huundwa kwa nazali, kipasuo pamoja na kiyeyusho ama cha ufizi /j/, au cha midomo /w/. Maneno yafuatayo yanashadidia maelezo hayo: *ngwenje*, *mbwembwe*, *gongwa*, *wambwa*, *mbwata na bingwa*. Hali hii huyashuritisha maneno ya mkopo katika Kiswahili kubadilika ili kuafikiana na mfumo wa fonolojia ya lugha hii (Mwita 2009).

Ifuatayo ni mifano ya mikakati ya urekebu wa kifonolojia katika Kiswahili:

5.1.2 Uchopekaji

Uchopekaji hutokea ili kuyapa maneno yaliyokopwa uwiano wa muundo wa silabi wa lugha ya Kiswahili. Katika Kiswahili, kama katika lugha nyingi za Kibantu, irabu huchopekwa katika mazingira ya kati ya shada ya konsonanti au mwishoni mwa neno ambalo halina irabu katika lugha chanzi ili kuhakikisha kwamba neno husika lina muundo pendwa wa silabi wazi na kurahisisha utamkaji. Hali hii hutokea katika mazingira ambamo neno la lugha chanzi halina silabi wazi, hali inayokinzana na uhalisia wa silabi za Kiswahili katika mchakato wa urekebishaji wa silabi (Batibo, 1996; Mwita, 2009; Iribemwangi, 2010).

Uchopekaji Fonimu katika Leksikoni zenye Asili ya Kiingereza

Ingawaje uchopekaji wa konsonanti hujitokeza katika maneno yaliyokopwa kutoka Kiingereza, uchopekaji wa irabu ndio ulio maarufu zaidi katika leksikoni zinazokopwa kutoka lugha hiyo:

Kiingereza	Kiswahili	Kiingereza	Kiswahili
<i>bundle</i>	bandali	<i>Tone</i>	toni
<i>gram</i>	gramu	<i>Judge</i>	jaji
<i>microphone</i>	maikrofoni	<i>Pipe</i>	paipu
<i>television</i>	televisheni	<i>Pump</i>	pampu
<i>aeroplane</i>	eroplani	<i>Dinosaur</i>	dinosau/dinosaria
<i>screw</i>	skrubu		

Ushahidi wa neno /skrubu/ hapo juu unadhihirisha kwamba hata konsonanti huweza kuchopekwa katika msamiati wa asili ya Kiingereza inapoingia katika Kiswahili.

Uchopekaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kiarabu

Maneno yaliyokopwa kutoka Kiarabu na kuingizwa katika Kiswahili pia yanaonesha uchopekaji wa irabu. Mkakati huu huhusisha ukiukaji wa kanuni ya uaminifu ili kufidia ukosefu wa fonifu yenza sawia katika lugha chanzi (Akida, 2009). Mifano ifuatayo ya msamiati ya Kiarabu inadhihirisha hali hii:

Kiarabu	Kiswahili	Kiarabu	Kiswahili
<i>qalam</i>	kalamu	<i>Alkhamis</i>	Alhamisi
<i>kitab</i>	kitabu	<i>Shahid</i>	shahidi
<i>muhasib</i>	mhasibu	<i>Albahr</i>	bahari
<i>mahkama</i>	mahakama	<i>Silah</i>	silaha

Uchopekaji Fonimu katika Leksikoni zenye Asili ya Kireno

Msamiati uliokopwa kutoka kwa Kireno pia inadhihirisha uchopekaji wa fonimu. Hali hii inabainika katika fonimu za irabu hasa lengo likiwa ni kupata muundo pendwa wa silabi. Zingatia mifano ifuatayo:

Kireno	Kiswahili
<i>fronha</i>	Foronya
<i>batata</i>	Mbatata
<i>sombreiro</i>	shumburere

Uchopekaji wa irabu /ɔ/ na /u/ katika maneno foronya na shumburere unakusudia kupata muundo pendwa wa silabi. Uchopekaji wa nazali ya midomo /m/ katika neno /mbatata/ unaelekea kutokea kinasibu tu kwani kuna maneno mengi ya Kiswahili ambayo yana muundo wa neno hilo katika lugha chanzi. Zingatia maneno kama *mbari*, *mbiu*, *mbeleko*, *mbati*, *mbawa* na kadhalika.

Uchopekaji Fonimu katika Leksikoni zenye Asili ya Kihindi

Uchopekaji wa fonimu katika maneno yenye asili ya Kihindi katika Kiswahili unajitokeza katika maneno machache kama ifuatavyo:

Kihindi	Kiswahili
<i>gond</i>	Gundi
<i>beroo</i>	Beberu
<i>rang</i>	Rangi
<i>ek bandook</i>	Bunduki
<i>jamaadaar</i>	jamedari

Kama inavyodhihirika katika neno *jamedari*, ni dhahiri kwamba uchopekaji wa irabu /i/ unaandamana na mabadiliko mengine yakiwamo ubadilishaji wa irabu /a/ pamoja na udhondoshaji wa wa irabu /a/.

5.1.3 Udondoshaji

Mkakati huu unaolenga kupata miundo sawa ya silabi inayoafiki ile ya lugha pokezi unahusu kuondolewa kwa irabu au konsonanti moja katika hali ambapo neno chanzi lina fonimu hizo kwa mfuatano (Madiba, 2000; Iribemwangi, 2008; Mwita, 2009; Njagi, 2016). Udondoshaji unajitokeza katika msamiati wa mkopo katika lugha ya Kiswahili kama inavyojitokeza hapa chini.

Udondoshaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kihindi

Msamiati wa asili ya Kihindi unabainisha udondoshaji wa irabu katika maneno:

Kihindi	Kiswahili
<i>ek bandook</i>	Bunduki
<i>saabun</i>	Sabuni
<i>dagala</i>	Dagla

Katika mifano hii, udondoshaji wa irabu /o/ na /a/ katika maneno *ek bandook* na *saabun* mtawalia, unaambatana na uchopekaji irabu /i/ mwishoni mwa maneno hayo. Ni vigumu kueleza udondoshaji wa irabu ya chini /a/ katika neno *dagla* kutoka *dagala* la Kihindi. Iitarajiwa kwamba neno hilo lingekopwa bila udondoshaji kwa kuwa lina muundo pendwa wa KI katika lugha chanzi, hali ambayo ingeafiki mfumo wa silabi wa lugha ya Kiswahili.

Udondoshaji wa silabi ya kwanza *ek* katika neno *ek bandook* unaandamana na mabadiliko mengine ya kifonolojia yakiwamo ubadilishaji wa irabu /a/ hadi /u/ na uchopekaji wa irabu /I/ mwishoni mwa neno hilo ili kupata muundo pendwa wa silabi katika Kiswahili.

Udondoshaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kiarabu

Maneno yaliyokopwa kutoka katika Kiarabu yanadhihirisha udondoshaji wa konsonanti zaidi kuliko irabu. Maneno mengi ya lugha ya Kiarabu huwa na shada ya konsonanti zenye sifa sawa kifonolojia. Konsonanti moja kati ya hizo zinazofuatana hudondoshwa ili kuleta uwiano katika Kiswahili (Akida, 2013).

Kiarabu	Kiswahili	Kiarabu	Kiswahili
----------------	------------------	----------------	------------------

<i>salat</i>	sala	<i>Aldawa</i>	dawa
<i>khatiya</i>	hatia	<i>Barakatih</i>	baraka
<i>Iiman</i>	imani	<i>Haqiqatan</i>	hakika

Maneno ya Kiarabu *aldawa* na *haqiqatan* yanadhihirisha udondoshaji wa silabi, kama ilivyobainika katika maneno yenye asili ya Kihindi hapo juu.

Udondoshaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kiingereza

Udondoshaji katika maneno yenye asili ya Kiingereza huhusisha konsonanti na irabu. Udondoshaji wa konsonanti hutokea katika maneno yenye konsonanti mbili zinazofuatana au pale ambapo konsonanti fulani haitamkiki. Aidha, neno lenye irabu isiyopatikana katika Kiswahili linapokopwa, huwa linafanyiwa urekebu kwa kudondosha irabu hiyo isiyo ya Kiswahili ili liafiki muundo wa silabi katika lugha ya Kiswahili. Tazama mifano ifuatayo:

Kiingereza	Kiswahili
<i>traffic</i>	Trafiki
<i>golf</i>	Gofu
<i>chalk</i>	Chaki
<i>commission</i>	Kamisheni
<i>committee</i>	Kamati
<i>lieutenant</i>	Luteni
<i>conole</i>	Kanali

Inatujuzu kutaja kwamba maneno haya yanapokopwa, ukopaji unalenga utamkaji wake katika lugha chanzi wala siyo othografia. Aidha, mifano ya maneno kama gofu na chaki unaonesha kwamba kitambaza /l/ ndiyo konsonanti inayodondoshwa mno katika msamiati wenye asili ya Kiingereza.

Udondoshaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kireno

Ingawaje lugha ya Kiswahili imekopa msamiati mchache kutoka Kireno, ushahidi unadhihirisha kwamba udondoshaji umejitokeza katika maneno yafuatayo:

Kireno	Kiswahili
<i>bendeira</i>	bendera
<i>trunfõ</i>	turufu
<i>cartãõ</i>	karata

Katika mifano hii, ni dhahiri kwamba irabu ndizo zinazodondoshwa maneno yanayokopwa kutoka Kireno. Aidha, kama ilivyo katika neno *turufu* ambalo asili yake ni /trunfõ/, nazali ya ufizi /n/ imedondoshwa kama sehemu ya sharti la kutimiza usawia wa miundo ya silabi za muundo pendwa wa KIKI katika lugha ya Kiswahili.

Udondoshaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kijapani

Msamiati wa asili ya Kijapani kwa Kiswahili, japo mchache, pia unadhihirisha udondoshaji. Zingatia maneno *jinriksha*, ambalo silabi ya awali *jin-* imedondoshwa neno hilo linapoingizwa katika Kiswahili na kuwa *riksho*. Udondoshaji wa silabi hiyo, umefungamana na ubadilishaji wa irabu /a/ kuwa /ɔ/ katika mazingira ya mwishoni mwa neno hilo katika Kiswahili. Hali hii inaelekea kuafikiana na utaratibu wa jumla katika lugha ya Kiswahili ambapo irabu hiyo ya nyuma /ɔ/ hutumiwa katika uundaji wa maneno yanayotaja vitu kama inavyodhihirika katika maneno kama *kifungo*, *kizibo*, *kiungo*, *muundo* na *windo* (Chisia, 2019).

5.1.4 Ubadilishaji

Ubadilishaji ni mkakati wa urekebu ambapo sauti fulani ya lugha chanzi inabadilishwa katika lugha pokezi ili kuwiana na mfumo wa kifonolojia wa lugha pokezi. Aghalabu sauti inayotumiwa katika lugha pokezi huwa na ukaribu kimatamshi na ile ya lugha chanzi (Mwita, 2009; Iribemwangi, 2013).

Ubadilishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kiarabu

Hali hii inadhihirika katika maneno yenye sauti za Kiarabu kama /x/, /q/ na /ħ/ ambazo zinakuwa /h/, /k/ na /h/ mtawalia, maneno hayo yanapoingizwaa katika mfumo wa Kiswahili. Mifano ifuatayo inaonesha haya:

Kiarabu	Kiswahili
<i>iqtisadi</i>	iktisadi
<i>Ḥarf</i>	herufi
<i>khamsini</i>	hamsini
<i>waqt</i>	wakati
<i>qahwa</i>	kahawa
<i>Ḥifadhi</i>	hifadhi

Mifano hii inaonesha kwamba ubadilishaji wa sauti za Kiarabu kama /q/, /kh/ na /ħ/ unakusudia kuleta uwiano wa kifonimu katika maneno ya Kiswahili.

Ubadilishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kireno

Ushahidi uliomo katika baadhi ya maneno yaliyokopwa kutoka Kireno unadhihirisha ubadilishaji wa fonimu za irabu na konsonanti. Hali hii inajitokeza katika irabu /ã/ kuwa /a/ na konsonanti /s/ ambayo inabadilika na kuwa /ʃ/, /ʒ/ au /z/. Aidha, irabu /ã/ inabadilika na kuwa /a/ ilhali /õ/ ibabadilika na kuwa /u/. Tazama mifano ifuatayo:

Kireno	Kiswahili
<i>sombreiro</i>	shumburere
<i>limãõ</i>	limau
<i>cartãõ</i>	karata

parafusō
mesa

parafujo
meza

Ubadilishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kiingereza

Ubadilishaji pia huhusisha irabu na konsonanti katika leksikoni zinakopwa kutoka Kiingereza na kuingizwa katika Kiswahili. Hali hii inabainika katika msamiati ufuatao:

Kiingereza
fashion
bicycle
bazooka
pistol
grenade

Kiswahili
fasheni
baiskeli
bazoka
bastola
gruneti/guruneti

Huku ikiwa rahisi kuelewa msingi wa ubadilishaji wa baadhi ya sauti za maneno yanapokopwa kutoka Kiingereza na kuingizwa katika Kiswahili, si rahisi kuelewa msingi wa ubadilishaji wa kipasuo sikhuna cha midomo /p/ hadi kipasuo ghuna cha midomo /b/ katika neno *bastola*, na ule wa kipasuo ghuna cha ufizi /d/ hadi kipasuo sikhuna cha ufizi /t/ katika neno *gruneti*.

5.1.5 Udumishaji wa Fonimu

Mkakati mwingine maarufu katika urekebu ni udumishaji. Hali hii hujitokeza pale ambapo msamiati unaoingizwa katika lugha fulani hudhihirisha sifa za kifonolojia za lugha chanzi. Kwa mfano, irabu au konsonanti za lugha chanzi huendelezwa katika lugha pokezi. Hali hii hutokea pale ambapo maneno husika yana sauti ambazo zinapatikana katika lugha zote mbili. Udumishaji wa fonimu ni mkakati ambao huhifadhi sifa za kifonolojia za leksikoni inayokopwa. Panaweza kutokea tofauti ndogo mno katika maneno hayo ambayo haileti tofauti kubwa katika msamiati husika (Batibo, 1996; Mwita, 2009; Iribemwangi, 2013).

Huku akijadili hali hii, Batibo (1996) katika Mwita (2009) anabainisha mambo matatu makuu ambayo yanaifanya lugha ya Kiswahili kudumishaa sifa nyingi za kifonolojia katika msamiati wake wa mkopo:

- i. Hali kwamba lugha ya Kiswahili imetagusana na Kiarabu, na hivi karibuni na Kiingereza (kuanzia karne ya 19) kwa kipindi kirefu.
- ii. Unyumbufu wake unaoiwezesha lugha hii kukopa msamiati wa asili ya kigeni
- iii. Umaarufu wake wa kutumia msamiati wa kigeni kwa kujinasibisha na utamaduni wa Kiarabu, na sasa Kiingereza.

Msamiati uliokopwa kutoka Kiarabu unadhihirisha udumishaji katika kiwango cha irabu na kile cha konsonanti. Hali hii inatokea pale ambapo sauti za lugha hiyo ya Kiarabu zina uwiano mkubwa na zile za Kiswahili (Mwita, 2009; Akida, 2013).

Tazama mifano hii:

Kiarabu	Kiswahili
<i>abjadīyah</i>	abjadi
<i>alfajr</i>	Alfajiri
<i>almaskan</i>	Maskani
<i>alhaju</i>	alhaji

Katika mifano hii, udumishaji wa shada ya konsonanti bj, lf, na nf unaambatana na udondoshaji katika neno *abjadi* na ubadilishaji katika *alhaji* na uchopekaji katika *alfajiri*.

Udumishaji wa shada ya irabu unabainika katika maneno yafuatayo yenye asili ya Kiarabu pia:

Kiarabu	Kiswahili
<i>Eali</i>	Aula
<i>Naam</i>	Naam

Udumishaji wa irabu katika maneno yanayokopwa kutoka Kiarabu kwenda Kiswahili siyo jambo jipya kwa kuwa lugha ya Kiswahili ina msamiati mwingi ambao unaonesha hali hiyo. Maneno yafuatayo yanadhihirisha hali hii: *uana*, *uuguzi*, *uaguzi*, *Uafrika*, *teua*, *iana*, *aoa*, *aua*, *aeua*, na kadhalika.

Udumishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kiingereza

Msamiati unaokopwa kutoka Kiingereza pia unadhihirisha udumishaji wa shada ya fonimu.

Kiingereza	Kiswahili
<i>albino</i>	albino
<i>alphabet</i>	alfabeti
<i>algebra</i>	algebra
<i>album</i>	albamu
<i>frame</i>	fremu
<i>fridge</i>	friji
<i>spanner</i>	spana
<i>tractor</i>	trekta
<i>trillion</i>	trilioni

Udumishaji wa konsonanti katika lugha ya Kiswahili ni hali iliyodumu. Hali hii ni bayana katika sauti mwambatano kama inavyojitokeza katika maneno yafuatayo: *fyeka*, *ndweo*, *vyakula*, *ugonjwa*, *mvulana*, *mvi*, *mbwembwe*, *ngwenje*, miongoni mwa mengine. Hata hivyo, taswira ya maneno kama *trekta*, *friji*, *baiskeli*, *teknoloji*,

albamu, albino na kadhalika, inadhihirisha mitindo mipya ya udumishaji katika lugha ya Kiswahili, hali inayoonesha unyumbufu wa lugha hii ya Kibantu.

Udumishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kireno

Msamiati unaokopwa kutoka Kireno pia unadhihirisha udumishaji wa shada ya konsonanti. Hali hii inahusisha shada ya konsonanti **mv** katika neno *mvinyo* na **nd** katika neno *bendera*. Hata hivyo, ni rahisi kuhitimisha kwamba hali hii inawiana na uhalisi wa taswira za maneno ya Kiswahili kama vile *mvi*, *mvulana* na *mvuvi*, pamoja na *nderemo*, *endelea* na *andika*. Hata hivyo, tunapotathmini neno *turufu* ambalo limetoholewa kutoka neno la Kireno *tunfō*, inaelekea kwamba irabu ya nyuma viringwa /u/ ilichopekwa kati ya nazali ya ufizi /n/ na kikwamizo sighthuna cha mdomo na meno /f/, hali inayoonesha kwamba ruwaza hiyo ya sauti haikubaliki katika maneno ya Kiswahili.

Kireno	Kiswahili
<i>kopo</i>	kopo
<i>bendeira</i>	bendera
<i>sombreiro</i>	shumburere

Katika mifano hii, ni dhahiri kwamba sauti zote katika neno kopo zimedumishwa, tofauti ya pekee ikiwa katika utamkaji. Maneno *bendera* na *shumburere* yanadhihirisha udumishaji wa nazali ya ufizi /n/ na kipasuo ya ufizi /d/, na nazali ya midomo /m/ pamoja na kipasuo cha midomo /b/ katika mifano ya pili na tatu hapo juu, hali ambayo inaafikiana na taswira ambayo ni ya Kiswahili, hasa maneno *mbele*, *mbuga*, *andama* na *mbilikimo* yakizingatiwa.

Udumishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kijapani

Msamiati uliokopwa kutoka Kijapani pia unadhihirisha udumishaji wa irabu. Tazama maneno yafuatayo:

Kijapani	Kiswahili
<i>jūdō</i>	judo
<i>kimōnō</i>	kimono

Mifano hii inadhihirisha udumishaji wa konsonanti na irabu ambapo tofauti ya pekee inajitokeza katika utamkaji.

5.2 Urekebu wa Kisemantiki

Urekebu wa kisemantiki ni mkakati wa urekebu ambapo maana za maneno yanayokopwa na kuingizwa katika lugha pokezi hufanyiwa marekebisho fulani. Utaratibu huu pia huchukua kipindi kirefu kufaulu. Urekebu wa kisemantiki unaainishwa katika matapo mbalimbali kutegemea athari za kimaana pamoja na fahiwa zinazofungamana na msamiati na istilahi zinazokopwa. Matapo hayo ni

pamoja na: uhamishaji wa kisemantiki, ubanaji wa kisemantiki, upanuzi wa kisemantiki, chuku, jazanda, uchukuaji fahiwa hasi na uchukuaji fahiwa chanya, miongoni mwa mengine (Akida, 2013; Mutwiri, 2020).

5.2.1 Uhamishaji wa Kisemantiki

Mkakati huu wa urekebu huhusisha hali ambapo maana ya kitu au dhana katika lugha pokezi huwahilishwa kutoka lugha chanzi kiasi kwamba maana hiyo ni tofauti na iliyotumiwa katika lugha chanzi. Katika utaratibu huu, maana mpya huwa na uhusiano wa karibu na ile ya lugha chanzi ila kitu au dhana ni tofauti katika lugha pokezi (Madiba, 2000; Akida, 2013; Iribemwangi, 2013; Njagi, 2016). Kinachosalia katika uhusiano wa maana mpya ya lugha pokezi na lugha chanzi ni chembe za uhusiano wa vitu au dhana husika.

Uhamishaji wa Kisemantiki wa Leksikoni zenye Asili ya Kireno

Msamiaji wa Kiswahili kutoka Kireno unadhihirisha uhamishaji wa kisemantiki. Neno *gereza* lilikopwa kutoka kwa *igreja* lenye maana ya *kanisa*. Uhamishaji wa kisemantiki hapa ulitokana na uhasama kutoka kwa Waarabu dhidi ya Wareno ambao uliwashurutisha Wareno kujenga makanisa yao ndani ya kuta kuu kama za gereza katika eneo la Mombasa. Uhamishaji huu wa kisemantiki unafungamana na kudhalilika kwa maana ambapo neno lenye fahiwa chanya, *igreja*, katika Kireno linachukua fahiwa hasi kwa sababu ya uhusiano wa uhasama kati ya makundi hayo mawili.

Uhamishaji wa Kisemantiki katika Leksikoni zenye Asili ya Kiarabu

Huku akitoa mifano kadhaa, ukiwamo wa neno la Kiswahili ‘ushuru’, Akida (2013) anasema kwamba maana ya neno asilia katika lugha ya Kiarabu ni ‘moja juu ya kumi’. Hata hivyo, maana ya sasa katika lugha ya Kiswahili ni ‘kodi inayolipwa kwa kuingiza bidhaa nchini’.

Mfano mwingine ni neno ‘husudu’ ambalo maana yake ni ‘penda mno; vutiwa mno na kitu, hali au mtu’. Neno hili limekopwa kutokana na nomino ‘husuda’ lenye maana ya ‘hali ya kutoyafurahia mafanikio au mali ya mwingine’. Ni bayana kwamba maana ya Kiarabu siyo inayotumiwa katika Kiswahili.

Neno *hakimu* (*Al-Hakim*) katika Kiarabu lina maana pana ya kiongozi wa ngazi ya juu katika taaluma au tasnia fulani kama mtawala, jaji au tabibu katika Kiarabu. Hata hivyo, katika Kiswahili neno hili *hakimu* lina maana moja tu: mwamuzi wa masuala ya kisheria mahakamani au ugomvi fulani.

Neno *hawara* katika Kiarabu lina maana ya ‘mdadisi au mtu anayependa kuuliza maswali kwa nia ya kufahamu mambo. Maana hii ni chanya na huenda ndiyo sababu neno hili linatumwa sana kama jina la watu wa kiume katika mataifa ya Uarabuni, hasa Misri. Hata hivyo, katika lugha ya Kiswahili, neno *hawara*

limebadilika kisemantiki na kuchukua fahiwa hasi katika utaratibu wa kusawajika kimaana au kudhalilika kwa maana (Masamba, 2004; Mutwiri, 2020). Katika lugha ya Kiswahili ‘hawara ni mwanamke anayewekwa na mwanamume bila kuolewa; kimada’.

Neno *kashfa* katika Kiarabu ni ‘kitenzi chenye maana ya kufichua kitu au hali’. Hata hivyo, maana inayotumiwa katika Kiswahili ya *kashfa* ni ‘tukio au jambo lenye aibu linalotokana na ukiukaji wa maadili’.

Katika Kiarabu neno *hadhi* linamaanisha ‘bahati’. Katika Kiswahili baada ya kukopwa neno hili limehamisha maana na kuwa ‘utukufu au heshima aliyo nayo mtu katika jamii kutokana na nafasi au cheo chake’. Ni dhahiri kwamba fahiwa yake imeimarika na kuwa bora.

Neno *jeneza* limekopwa kutoka Kiarabu likiwa na maana ya ‘matanga’. Hata hivyo, maana yake imehamishwa katika Kiswahili na kuwa ‘sanduku linalotumiwa kumzika marehemu’.

Aidha neno *itifaki* lililokopwa kutoka Kiarabu likiwa na maana ya ‘mkataba au makubaliano’ limeshuhudia uhamisho wa kisemantiki katika Kiswahili kwa kuwa katika lugha hii neno hilo linamaanisha ‘taratibu za kiserikali zinazoshughulikia masuala rasmi; protokali’.

Uhamishaji wa Kisemantiki katika Leksikoni zenye Asili ya Kiingereza

Utafiti wetu unabainisha mifano ya uhamisho wa kisemantiki kadhaa katika leksikoni zilizokopwa kutoka lugha ya Kiingereza. Tataeleza baadhi ya mifano hiyo hapa chini:

Neno *simu* linatokana na neno *sim* ambalo maana yake ni ‘kadi inayotiwa katika kifaa cha mawasiliano kama rununu inayohifadhi habari mahususi za mmiliki wake kama nambari ya utambulisho, nambari ya rununu na arafa’. Baada ya kuingizwa katika lugha ya Kiswahili neno hili linatumiwa kwa maana ya ‘kifaa cha mawasiliano ambacho kina uwezo wa kurusha sauti mbali’. Urekebu huu unafungamana na utaratibu wa kiistiari ambapo fahiwa ya lugha pokezi inahusishwa moja kwa moja na kadi katika lugha chanzi.

5.2.3 Upanuzi wa Kisemantiki

Upanuzi wa kisemantiki ni mkakati wa kulipa neno linaloingizwa katika lugha fulani maana zaidi ya ile ya lugha chanzi.

Ushahidi wa upanuzi wa kisemantiki unadhihirika katika leksikoni ‘karata’ iliyokopwa kutoka Kireno. Neno hili katika Kireno lina maana ya kadi ya kuchezea iliyo na tarakimu na michoro. Katika lugha ya Kiswahili, mbali na maana hiyo tuliyotoa hapo juu, neno hili hutumiwa katika nahau ‘cheza karata’

kwa maana ya kupambana au kukabiliana na jambo kwa ustadi. Urekebu huu unafungamana na utaratibu wa kiistiari ambapo maana ya lugha chanzi inasawiriwa katika maana zote mbili za lugha ya Kiswahili.

5.2.4 Ubanaji wa Kisemantiki

Ubanaji wa kisemantiki ni mkakati wa urekebu ambapo maana ya neno linalokopwa hupewa umahususi wa kimaana katika lugha pokezi. Katika mkakati huu neno katika lugha chanzi linaweza kuwa na maana pana kiasi cha kurejelea hali na dhana mbalimbali. Hata hivyo, maana yake hubanwa kiasi cha kurejelea hali na dhana mahususi na finyu katika lugha pokezi. Uhusiano huu huitwa pia *sinedoche* (Fromkin, 2003; Akida, 2013; Mutwiri, 2020).

Ubanaji wa Kisemantiki katika Leksikoni zenye Asili ya Kiingereza

Leksikoni zilizokopwa kutoka Kiingereza zinadhihirisha ubanaji wa kisemantiki. Neno ‘profesa’ linatumiwa kumtaja mhadhiri au mwalimu wa ngazi na tajiriba ya juu katika chuo kikuu katika Kiingereza na Kiswahili. Hata hivyo, neno hilo linatumiwa kumtaja mfuasi wa kitu, imani au itikadi fulani katika Kiingereza. Maana hii ya pili haitumiwi katika Kiswahili.

Maneno mengine ni pamoja na ‘benki’. Katika Kiingereza neno benki lina maana ya:

- i. Mahali panapohifadhiwa na kutolewa fedha.
- ii. Tendo la kuweka pesa katika akaunti.
- iii. Hifadhi ya vitu vinavyoweza kutumiwa vikihitajika.
- iv. Hifadhi vitu kama manii au damu kwa matumizi ya baadaye.
- v. Tegemea mtu au kitu kwa jambo fulani.

Katika lugha ya Kiswahili, neno ‘benki’ lina maana moja tu: mahali panapohifadhiwa na kutolewa fedha.

Soda, katika Kiswahili na Kiingereza, ni kinywaji kitamu kisicholevya kinachoundwa kwa sukari, maji, aina fulani ya kemikali na gesi maalumu.

Hata hivyo, katika Kiingereza *soda* pia ni kinywaji fulani chenye mapovu ambacho aghalabu huchanganywa na pombe.

Neno ‘teksi’ lenye asili ya Kiingereza *tax* lina maana ya gari dogo la kukodi au kukodisha kwa usafirishaji wa watu au mizigo. Katika lugha ya Kiingereza neno hili lina maana tatu:

- Gari dogo la kukodisha au kukodi kwa usafirishaji wa watu au mizigo
- Tendo la kutumia gari dogo la kukodi au kukodisha kwa usafiri
- Tendo la ndege kusonga polepole katika njia yake kabla ya kupaa angani

Neno ‘hospitali’ linalotokana na neno la Kiingereza *hospital* lina maana tatu:

Taasisi inayotoa huduma za matibabu, upasuaji pamoja na uuguzi kwa wagonjwa.

Taasisi ya ukarimu kwa wachochole, wakongwe, wagonjwa, au watoto.

Makao yanayotoa huduma za uangalizi kwa wagonjwa, hasa wanaoelekea kufariki.

Katika Kiswahili, neno hili ‘hospitali lina maana moja tu: taasisi inayotoa huduma za matibabu, upasuaji pamoja na uuguzi kwa wagonjwa.

Neno *budget* la lugha ya Kiingereza kwa Kiswahili ‘bajeti’ linatumiwa kama nomino na kitenzi, tofauti ikiwa katika mkazo. Maana hizo ni:

Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za serikali, mtu au kampuni.

Kutengeneza makadirio ya mapato na matumizi ya serikali, mtu au kampuni.

Katika lugha ya Kiswahili, maana ya neno hili ‘bajeti’ imebanwa kiasi cha kutumiwa kama nomino tu, yaani ‘makadirio ya mapato na matumizi ya serikali, mtu au kampuni’.

Neno ‘kampuni’ lenye asili ya Kiingereza, yaani *company* lina maana sita katika lugha hiyo ila maana mbili tu katika Kiswahili. Katika lugha chanzi neno hili lina maana zifuatazo:

Shirika la kibiashara;

Kikundi cha askari au maskauti ambacho ni kidogo kuliko kikosi.

Hali ya kuwa na mtu au watu, au mtu/watu alio nao mtu.

Kikundi cha waigizaji, waimbaji au wacheza dansi wanaofanya shughuli zao pamoja.

Kikundi cha ndege hasa batamwitu aghalabu zaidi ya elfu moja.

Kujihusisha na mtu au watu.

Katika lugha ya Kiswahili, neno hili lina maana mbili tu, hizo tulizoeleza hapo juu za kwanza mbili. Isitoshe, ni bayana kwamba katika matumizi ya wengi, maana ya kwanza, yaani ‘shirika la kibiashara’ ndiyo inayozingatiwa.

Katika mifano hii, inadhihirika kwamba ubanaji wa kisemantiki unaohusisha leksikoni za asili ya Kiingereza hulenga nomino zaidi. Maana ya vitenzi haikopwi ila tu hujitokeza leksikoni hizo zitumiwapo katika nahau kama ‘unda bajeti’, ‘laza hospitalini’ na ‘amua kesi’.

Ubanaji wa kisemantiki katika Leksikoni zenye Asili ya Kiarabu

Msamiati wa Kiswahili uliokopwa kutoka Kiarabu unadhihirisha ubanaji wa kisemantiki. Hali hii inabainika katika mifano ifuatayo:

Neno	Kiarabu	Kiswahili
hamu	1. tamaa/ari ya kupata kitu. 2. shauku/dhiki/majonzi	ari/tamaa ya kupata kitu
kadhi	1. jaji/hakimu 2. jaji/hakimu wa kidini (Uislamu)	jaji/hakimu wa kidini (Uislamu)
ghali	1. -enye bei/thamani ya juu 2. kipenzi/mpenzi	-enye bei/thamani ya juu
harakati	1. juhudi/jitihada 2. kusongasonga kutoka eneo moja hadi jingine	juhudi/jitihada

Ubanaji katika Msamiati wenye Asili ya Kijapani

Neno *karate* lina maana mbili katika Kijapani: ‘mikono mitupu’ na ‘maarifa au mchezo wa kujikinga kwa kutumia mikono au miguu bila silaha’.

Katika Kiswahili, neno hilo lina maana moja tu ya ‘maarifa au mchezo wa kujikinga kwa mikono na miguu bila silaha’.

5.2.5 Udumishaji wa Kisemantiki

Katika mkakati huu, maana ya neno katika lugha chanzi huhifadhiwa hata baada ya kukopwa na kuingizwa katika mfumo wa lugha pokezi. Mabadiliko ya kimatamshi au hata kiothografia yaweza kulipata neno au istilahi husika ila maana husalia ileile ya lugha chanzi. Mkakati huu hudhihirika mno katika msamiati wa kawaida kuliko katika istilahi (Madiba, 2000).

Udumishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kiingereza

Udumishaji wa kisemantiki unajitokeza katika msamiati ufuatao wenye asili ya Kiingereza:

Neno	Kiingereza	Kiswahili
vocha	fomu ya malipo yenye taarifa za jina, pesa na sababu za malipo	fomu ya malipo yenye taarifa za jina, pesa na sababu za malipo.
motokaa	gari linaloenda kwa kutumia injini	gari linaloenda kwa kutumia injini
dijitali	-enye kutumia mfumo wa dijiti.	-enye kutumia mfumo wa dijiti.
dikteta	kiongozi wa kiimla	kiongozi wa kiimla.
dereva	mtu anayeendesha gari, treni au trekta	mtu anayeendesha gari, treni au trekta

Udumishaji katika Leksikoni zenye Asili ya Kireno

Udumishaji wa kisemantiki unajitokeza katika neno *turufu* lililoingizwa katika lugha ya Kiswahili kutoka Kireno. Kama ilivyo katika Kireno, neno hili lina maana tatu katika lugha ya Kiswahili ambazo ni: mosi, karata ambayo haiwezi

kuongoza hata mzunguko mmoja; pili, karata yenye nguvu nyingi; na tatu, kauli au uamuzi wa mwisho kuhusu jambo.

6.0 Hitimisho

Utafiti wetu umebaini kwamba lugha ya Kiswahili, kama lugha nyinginezo zenye matumizi mapana katika jamii, inaendelea kukua ili kuyafanikisha mawasiliano yote, yakiwamo mawasiliano rasmi nchini Kenya. Tumezingatia mikakati miwili mikuu: matumizi ya Kiswahili na upanuzi wa msamiati kupitia ukopaji na utohozi. Utafiti huu umebainisha kwamba lugha ya Kiswahili inatumiwa katika mawanda mbalimbali kama vile ya elimu, bunge la kitaifa na vyombo vya habari. Hata hivyo, matumizi ya Kiingereza yako kwa kiasi kikubwa mno katika mawanda hayo kutokana na hamasa ya kiutekelezaji ambapo wengi wanakihusisha na fursa nyingi na muhimu za kujiendeleza kiuchumi, kiusomi na kitaaluma, pamoja na dhana kwamba lugha hiyoya Kiingereza inahusishwa na taashira nyingi za kimataifa. Aidha, utafiti wetu umebainisha ukopaji na utohozi kama mikakati ambayo Kiswahili kinatumia katika kuasilisha msamiati na istilahi. Katika kukopa, wataalamu wengi wanasisitiza mkabala wa uhasilia. Utafiti huu umebainisha kwamba ukopaji na utohozi unafungamana na mikakati mbalimbali ya urekebu wa kifonolojia na kisemantiki ili kuafiki mahitaji ya kiisimu ya lugha ya Kiswahili. Ushahidi umeonesha kwamba licha ya kukopa mno kutoka Kiarabu, lugha hii inakopa mno msamiati na istilahi za elimu, mawasiliano, sayansi na teknolojia katika lugha ya Kiingereza katika enzi hizi.

Marejeleo

- Akida, M.A. (2013) "Phonological and Semantic Change in Language Borrowing: The Case of Arabic words Borrowed into Kiswahili". *International Journal of Education and Research*. Juz. 1(2) uk.1-20
- Coulmas, F. (1989) "Language Adaptation". Katika F. Coulmas (mh.) *Language Adaptation*. New York: Cambridge University Press. Kur. 1-25
- Iribemwangi, P.I. (2012) "The Global Place of Kiswahili: Yesterday, today and tomorrow." Katika P.P. Gichana, P.I. Iribemwangi na C. Onsare (Wah.) *English-Kiswahili Learner's Handbook*. Nairobi: Petersberg International Publishers. kur. 11-16.
- Iribemwangi, P.I. na Mukhwana, A. (2011) *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers.
- Ketzer, M.M na Oluoch-Sule, E. (2022) "Hidden Potentials for African Languages in Curriculum Reforms: Examples from Kenya and South Africa". *SN Social Sciences*. <https://doi.org/10.007/543545-022-00440-6> . Ilisomwa tarehe 10 Agosti 2024.
- Madiba, M.R. (2000) *Strategies in the Modernisation of Venda*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Afrika Kusini.

- Massamba, D.P.B. (1989) "An Assessment of the Development and Modernization of the Kiswahili Language in Tanzania". Katika F. Coulmas (Mh.) *Language Adaptation*. New York: Cambridge University Press.
- Michira, J.N. na Iribemwangi, P.I. (2014) "Kiswahili as an Official Language in Kenya: It's Past, Present and Future Roles and Challenges". *Reyono: Journal of Interdisciplinary Studies*. Juz. 3(1): 42-52.
- Monitor, G.L. (2017) "Global Language Monitor. Kutoka Number of Words in the English Language". Katika <https://www.languagemonitor.com/global-English/number-of-words-in-the-english-language-10.41257-5>
- Musau, P.M. (2002) "Language Attitudes and their Implications for Language Planning in Kenya". *International Journal of the School of Humanities and Social Sciences*. Juz. 2 (1): uk. 93-105
- Mutwiri, T.G. (2020) *Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Mtazamo Linganishi wa Kikale na Kisasa*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mwita, L.C. (2009) "The Adaptation of Swahili Loanwords from Arabic: A Constraint-Based Analysis. *The Journal of Pan African Studies*. Juz. 2 (8)uk. 46-61
- National Assembly of Kenya (2022) *Fact Sheet 2: The Legislative Process*. Nairobi: The Clerk of the National Assembly.
- Njagi, J.K. (2016) *Lexical Borrowing and Semantic Change: A Case of English and Gikuyu Contact*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Oduor, J. na Timammy, R. (2016) "The Treatment of Kiswahili in Kenya's Education System". *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics*, Juz. Na. 5: 174-194.
- Ojwang, B. (2011) "Political and Sociolinguistic Obstacles to the Expanded Functions of Kiswahili in Kenya". *Language Matters*, Juz. 42 (2): 231-247.
- Okombo, D.O. (2001) *Language Policy: The Forgotten Parameter in African Development and Government Strategies*. Nairobi: University of Nairobi.
- Onyango, J.O. (2005) "Issues in National Language Terminology Development in Kenya". *Swahili Forum*, Juz. 12: 219-234.
- Republic of Kenya (2010) *The Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Printer.
- Wamitila. K.W. (2016) *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. Nairobi: Vide-Muwa.